# APTNESS CONSULTANCY

TAX |ACCOUNTING| ADVISORY


# UKAGUZI WA KODI (TAX EXAMINATION)



# 1. UKAGUZI NI NINI?.

- Ukaguzi wa kodi ni mchakato unaofanywa na mamlaka ya mapato ili kuhakikisha walipa kodi (mlipa kodi) ametoa taarifa sahihi kuhusu mapato yake, matumizi na kiasi cha kodi anachopaswa kulipa kulingana na sheria za kodi

- Hufanyika na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuhakikisha kuwa mlipa kodi amelipa na kuripoti kodi kwa usahihi.  Sheria ya usimamiaji wa kodi(Tax administration Act) inaruhusu TRA kufanya ukaguzi hadi miaka mitano iliyopita, isipokuwa ikiwa kuna viashiria vya udanganyifu vinavohitaji muda mrefu zaidi.



# 2. AINA ZA UKAGUZI WA KODI

- **Ukaguzi wa Kawaida (Tax Examination)**

Huu ni ukaguzi wa awali ambao uhusisha mapitio ya nyaraka za kodi na taarifa za kifedha.

TRA utumia taarifa walizo nazo tayari kama Marejesho ya Ritani, Risiti za EFD, Taarifa za Kibenki n.k.

- **Ukaguzi wa Kina (Tax Audit)**

Huu ni Mchakato wa kuchunguza kwa kina taarifa za mlipakodi ili kuthibitisha mapato na kodi iliyolipwa. Aina hii ya ukaguzi hufanywa kwenye eneo la mfanyabiashara(Field audit)

# AINA ZA UKAGUZI WA KODI cont....

- **Ukaguzi wa kiuchunguzi (Tax Investigation)**

Ni uchunguzi wa kina zaidi wa taarifa za mlipa kodi ambao unafanywa pale ambapo TRA inawasiwasi, ushaidi wa udanganyifu ,uhalifu wa kodi. Hii ufanywa bila taarifa ya awali.

Aina hii ya ukaguzi unaweza kupelekea mteja kupelekwa mahakamani kwa makosa ya jinai kama;

- Kutumia risiti feki au EFD zisizo halali.
- Kuficha mapato kwa makusudi.
- Uwasilishaji wa taarifa za uongo.

# AINA ZA UKAGUZI WA KODI cont…

TRA inaweza kushirikiana na wapelelezi wa kiserikali na mamlaka nyinginezo za kisheria kukamilisha uchunguzi. Baada ya uchunguzi kukamilika inaweza kupelekea faini kubwa, kifungo au vyote kwa Pamoja.

- **ukaguzi wa VAT (VAT verification)**

Huu ni uhakiki wa taarifa za VAT zilizo wasilishwa TRA na wateja waliosajiriwa kuisaidia serikali kukusanya kodi ya Ongezeko la thamani. Aina hii ya ukaguzi TRA wanahakiki mauzo na manunuzi yaliyofanyika na Mlipakodi kama yanakidhi vigezo.



# 3. LENGO LA UKAGUZI WA KODI



- Kuthibitisha usahihi wa taarifa za kodi zilizowasilishwa na mlipa kodi.
- Kubaini udanganyifu na mapungufu ( Errors & frauds)
- Kukusanya kodi inayodaiwa ikiwa kuna mapungufu yamebainika.

# 4. SABABU ZA UKAGUZI NI ZIPI?

Zifuatazo ni sababu zinazopelekea TRA kufanya ukaguzi/ kuchagua mlipakodi wa kumfanyia ukaguzi. (Section 45 of Tax administration Act CAP. 438 R.E 2019 reading together with the Finance Acts).

- ❖ Aina ya biashara. mfano, ujenzi, biashara ya fedha taslimu.
- ❖ Vigezo vya Sekta. Mfano, Sekta ya madini
- ❖ Vigezo vya kanda. kanda zenye walipa kodi wenye kipato zaidi.
- ❖ Kutofautiana kwa Taarifa.
- ❖ Kuripoti hasara kwa miaka mfululizo.
- ❖ Kutolipa au kuchelewa kulipa kodi.
- ❖ Taarifa za mtu wa tatu (Third party information).

Iwapo mtu amekaguliwa au kuchunguzwa kwa kipindi fulani, ukaguzi/uchunguzi huo hautamzuia mtu huyo kukaguliwa au kuchunguzwa katika kipindi kinachofuata ikiwa kuna sababu za msingi za kufanya hivyo

# 5. VITU GANI UKAGULIWA?

- Taarifa za mapato na Matumizi
- Risiti na stakabadhi za malipo
- Rekodi za miamala ya kibenki (Bank Statements)
- Mikataba ( Pango, wafanyakazi).
- Mishahara na kodi za wafanyakazi.



# 6. MAPUNGUFU YANAYOWEZA KUONEKANA WAKATI WA UKAGUZI

- Kutowasilisha Ritani za kodi (VAT , PAYE, SDL WHT na Income Tax )
- Mapato yaliyofichwa ( Undereporting of income)
- Matumizi yasioeleweka (Unsupported expenses)
  - -Gharama ambazo hazina vielelezo (Risiti)
  - - Matumizi binafsi kuonyeshwa kama matumizi ya biashara
- Kutokuweka kumbukumbu sahihi za kifedha.
  - - kukosa vitabu vya hesabu na taarifa zisizokamilika
  - - Matumizi ya risiti bandia, zisizoeleweka.

# MAPUNGUFU YANAYOWEZA KUONEKANA WAKATI WA UKAGUZI cont…

- Taarifa zinazokinzana – Benki na Hesabu, Kutofautiana kwa mauzo yaliyokipotiwa kwenye mfumo wa TRA (EFDMS) na EFD.

# 7. MAMBO YA KUZINGATIA KWENYE UKAGUZI

1. **KABLA YA UKAGUZI**

i. Andaa nyaraka zote muhimu. Taarifa za kifedha(cash book, ledger, balance sheet and Income statement), Risiti za mauzo na matumizi, Bank statements, Nyaraka za uthibitisho wa malipo ya kodi (VAT, PAYE,WHT n.k), Mikataba ya biashara.

ii. Taarifa za kodi Zilingane (TRA na vitabu)

iii. Uhalali wa matumizi . Matumizi yanafanane na biashara inayofanyika pia yawe na vielelezo kamili.(Vouchers, invoice, proof of payments)

iv. Husisha wahasibu na washauri wa Kodi

# MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UKAGUZI cont…

2. **WAKATI WA UKAGUZI**

i. Toa ushirikiano

ii. Jibu maswali kwa uangalifu, usitoe taarifa za kubahatisha, kama huna uhakika omba muda wa kuangalia na kupitia kwa umakini.

iii. Omba ufafanuzi kabla ya kusaini nyaraka yeyote.

# MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UKAGUZI cont…

**3. BAADA YA UKAGUZI**

i. Pitia ripoti ya ukaguzi kwa umakini.

ii. Wasilisha pingamizi ikiwa hukubaliani na matokeo ya ukaguzi – Ndani ya siku 30 ( file the Objection on the issued assessment).

iii. Lipa kodi unayodaiwa kama huna pingamizi. Unaweza kuomba kulipa kwa awamu kama kodi ni kubwa.

iv. Boresha mifumo yako ya kiuhasibu. Unaweza kupata msaada kutoka kwa Washauri wa kodi ( Tax consultants) ili kupunguza makosa.

# 8. HATUA ZA UKAGUZI WA KODI

1. Notisi ya Ukaguzi.

- Mamlaka ya Mapato TRA humjulisha mlipakodi kwa maadishi kuhusu ukaguzi wa biashara yake, Ujumbe huo utaonyesha siku na muda wa ukaguzi. Mlipa kodi anaruhusiwa kuomba kwa maandishi kusogezewa muda wa ukaguzi kama anasababu ya msingi.

2. Maandalizi ya ukaguzi.

- TRA wanaweza kabla ya ukaguzi wakampatia Mlipa kodi orodha ya vitu vinavyohitajika kwajiri ya ukaguzi. Mfano, nyaraka za hesabu, Mikataba n.k

# HATUA ZA UKAGUZI cont…

3. Ukaguzi halisi.

- TRA ufanya ukaguzi wa nyaraka na taarifa za kifedha za mlipakodi, wataangalia uhalali wa taarifa zilizowasilishwa kwenye hesabu kwa kupitia kuhusianisha na nyaraka mbalimbali zilizopo, ikiwemo Risiti za EFD, mikataba , n.k

4. Kuwasilisha matokeo ya ukaguzi( Audit Findings).

-TRA atawasilisha kilichoonekana kwenye ukaguzi ambapo Mlipakodi atapewa nafasi ya kutoa maelezo ya matokeo ya ukaguzi kama anapingamizi au hoja kuhusu matokeo ya ukaguzi.

5. Ripoti ya ukaguzi.

- Ripoti ya ukaguzi itaonyesha taarifa zilizokaguliwa, mapungufu, makosa yaliyogunduliwa na Kodi ya kulipa kama ipo

# HATUA ZA UKAGUZI

Mlipa kodi anahaki ya kupinga kama hajaridhika, atawasilisha pingamizi lake TRA ndani ya siku 30 kutoka siku madai ya kodi ya kulipa yametoka.

Mwisho...

# APTNESS CONSULTANCY

TAX |ACCOUNTING| ADVISORY